

## **BALENZI**

### **E. Kezilahabi**

Watoto kijijini walizoea kumwita "Mzee Zikambona". Jina hili alipewa na wanakijiji. Hili ni jina ambalo hupewa mtu mwenye ukiwa ambaye amefikwa na maafa mfululizo. Mkewe aliitwa na watoto "Nyokonyoko" ingawa jina na alilopewa na wanakijiji tangu siku ya arusi lilikuwa Balenzi. Mapenzi na mshikamano ya hawa wazee wawili yaliwashangaza wanakijiji. Walikuwa hawajapata kuona mapenzi ya izeeni ya aina hii. Kila Jumamosi asubuhi watoto jirani walizoea kwenda nyumbani kwa Mzee Zikambona kusubiri sanaa yao ya maonyesho. Mzee Zikambona hakuwfukuza kwa sababu alijua walisaidia kumliwaza mkewe, Balenzi. Wanakijiji pia walifikiri hivyo.

Jumamosi hii watoto walimkuta Mzee Zikambona akivuta kiko chake chini ya kivuli cha mchungwa. Watoto walifika mapema kidogo kwa sababu ng'ombe wake alikuwa amezaa na walitegemea chai ya maziwa na viazi vitamu. Hawakukosea. Si muda mrefu Balenzi alitoka nje na vikombe vyta plastiki vyenye chai ya maziwa. Walimsalimu kwa adabu na kumpokea, kisha watoto wawili walikwenda naye ndani ya nyumba na kurudi na sahani tatu zenyet na viazi vitamu. Balenzi, akiwa mwenye tabasamu aliwafuata nyuma akiwa na kikombe cha mmewe. Alimwekea mezani kwa heshima akarudi ndani na kuchukua kikombe chake na kiti. Wakaanza kunywa chai ya asubuhi.

"Kunyweni wanangu," Balenzi aliwambia watoto.

"Balenzi," alianza mumewe baada muda mfupi wa kimya

"Mume wangu," aliitikia mkewe.

"Ile ndege ya jana hukuiamini?"

"Mume wangu! Mwili wangu unajua siku na mlion ulioleta kilio na majonzi."

"Mama!" mtoto mmoja alidakia, "hizo ndizo ndege za kisasa. Zinaitwa jeti. Zinaruka juu sana hata mlion hauwezi kusikika. Ila moshi unaofuata nyuma ndio unaonishangaza."

"Nasikia zinaruka juu kwa sababu zinaogopa kupigwa na manati," mtoto mwininge alidakia.

Mazungumzo ya watu wazima – mazungumzo yaliyoweza kung'oa moyo na mizizi yake – yakawa yametekwa na watoto. Huyu anasema hili na mwininge lile. Baada ya muda kukawa na ukimya.

"Alisema miaka hamsini ya ndoa yetu angetununulia gari," Zikambona alianza tena.

"Wakati huo tungelionyesha mapengo yetu kwenye madirisha ya gari. Tungekuwa watu wa kutazamwa tukatazamika."

"Hiyo ndiyo ingekuwa tabasamu yetu ya maisha."

Kimya.

“Jino langu jingine limeanza kutingishika,” alisema Balenzi.

“Tazama!” mtoto mmoja wa kike alisimama kwenda kumwonyesha Balenzi.

“Tazama, jino hili linatingishika. Mengine yameng’oka. Hivi kweli yataota tena?”

“Yataota mazuri zaidi,” Balenzi alimhakikishia. Watoto wengine walianza kueleza jinsi meno yao yalivivotupwa juu ya paa la nyumba ili mengine yaote haraka. Walianza kuonyeshana meno. Mazungumzo yakawa yamekatishwa tena.

Kimya.

“Balenzi.”

“Mume wangu.”

“Naona kama mchungwa huu hautatoa matunda mwaka huu.”

Áh! Mume wangu, Mwaka huu mvua zimekawia. Lakini nahisi mvua itanyesha usiku wa leo. Mvua zikikawia namna hii huja na upepo mwingu na mafuriko.”

Kimya.

Ghafla Balenzi alianza kutetemeka mwili mzima. Alianza kupiga kelele kama mtu aliyepagawa. “Ninamwona! Huyo! Yumo ndani ya ndege! Ninamwona!” Watoto walismama tayari kwa mbio zao za kila wiki. Mzee Zikambona alimtazama mkewe kwa huruma. Mlio wa ndege ulianza kusikika. Ulikaribia. Balenzi alitazama juu angani. Akaiona ikipita juu ya mji wao. Alianza kufukuzana nayo hali akipiga kelele, “Nyoko! Nyoko!” Alikuwa akiinyooshea kidole. Watoto walimfuata nyuma mbio wakimuunga mkono, “Nyoko! Nyoko!” hadi ndege ilipopotea na mlio wake kutosikika tena. Walirudi nyumbani na kumkuta Mzee Zikambona akiwafukuza kuku waliokuwa wakishambulia viazi vilivyoachwa juu ya sahani.

“Leo mmepiga kelele, nafikiri hata rubani amewasikia.” Mzee Zikambona aliwambia. Walicheka. Balenzi alitabasamu. “Wamezoeal! Hivi, hiki kijidege chao hakizeeki wakakoma kupita hapa!” alisema Balenzi.

“Hiyo ni ndege iletayo magazeti na barua. Balenzi, ambacho hakizeeki ni majonzi yetu.”

Watoto walimalizia chai. Kabla hawajaondoka Mzee Zikambona alimwambia mtoto mmoja, “Kaniletee enanga yangu ndani ya nyumba. Natema mate urudi kabla hayajakauka. Mtoto alikwenda mbio. Huku nyuma Mzee Zikambona alichukua mchanga kidogo akautupia juu ya mate. Mtoto alirudi mbio.

“Yamekaukia!”

“Zamani!” Mzee Zikambona alijibu. Mtoto aliyatazama akacheka “Mzee mjanja huyuu!” Watoto wengine walicheka. Wakaondoka kuelekea makwao.

Walipokuwa wamekwenda, Mzee Zikambona alianza kupiga wimbo wake wa tuni ujulikanao kama “Omuhyomolo.” Baada ya hapo alipiga wimbo ambao Balenzi alikuwa hajausikia. Ulikuwa wimbo mpya. Aliimba:

Panzi huruka na mpenziwe  
Kama chombo cha anga  
Njia na barabara akavuka  
Salama akatua  
Majanini upande wa pili  
Macho ya ndege akiepuka  
Na midomo na kwato za ng'ombe  
Wachungao akipisha  
Ingawa hawezu dunia kuzunguka  
Au Mwezini kutua  
Maisha ya wawili ni kama.

Chatu mpenziwe akifa  
Hujinyima kula hadi kufa  
Na njiwa hufa kwa huzuni  
Sokwe wiki maiti huchunga  
Harufu asijali.  
Maisha ya wawili si kama.

Wewe na mimi  
Tuhesabu nyota  
~~Hadi~~ tutaposahau  
Tulipofikia  
Na kuanza upya.  
Tena na tena, mbili milele  
Salama tutatua upande wa pili.

“Mume wangu,” Balenzi alimwambia mmewe baada ya kuurudia mara ya tatu.

“Mbona umeanza kufikiria mazito mwenzangu.”

“Huu wimbo niliutunga baada ya kuona kumbikumbi wawili wakifuatana wiki iliyopita. Mara nyingi nimeona panzi wawili mmoja juu ya mwingine.” Mzee Zikambona alipiga nyimbo zingine tatu ambazo zilikuwa zikijulikana sana kijijini. Baada ya hizo nyimbo Balenzi alichukua jembe, akaaga kwenda kuchimba mihogo. Huku nyuma Mzee Zikambona alileta mkeka, akakunja blanketi kama mto, akalala usingizi wa adhuhuri. Yote yalikuwa wazi.

“Hamwezi kumpitisha Bibi Arusi wenu hapa mpaka kwanza miereka ipigwe. Tukiwashinda huyu Bibi Arusi hatoki humu kijijini.” Maneno haya yalisemwa na kijana mmoja mwenye kifua kipana na mzito. Walikuwa kwenye mpaka wa kijiji. Walijua haikuwa utani. Ilikuwa jadi. “Yaani ninyi watoka mbali mmetudharau sana ee!” aliendelea. “Mnafikiri kijini chetu hakina wavulana wa kumwoa huyu binti!”

“Wanaume gani ninyi mmezubaa mpaka sisi wanaume halisi tukaja!” alijibu mapigo kijana mmoja kutoka kwenye kundi lenye Bibi Arusi. Vijana watano walichaguliwa kutoka kila upande. Bibi Arusi alikalishwa kwenye

kivuli. Vijana waliochaguliwa walianza kujigamba wakitifua mchanga na kuzungusha shingo zao kama madume ya ng'ombe. Walikubaliana ziwe raundi mbili mbili kwa kila watu wawili. Miereka ilianza. Kila aliyewekwa kisogo chini wimbo wa majigambo na kejeli uliimbwa na walioshinda. Miereka iliendelea hadi jua lilipokaribia kutua. Hapo ndipo wenyenye Bibi Arusi walipoingiza uwanjani mabingwa wao wawili wa mwisho. Walikuwa mabingwa hasa. Vijana waliotoka kijiji na Bibi Arusi walitupwa chini kama magogo ya miti hata Bibi Arusi akasahau kwao akashangilia alikoolewa. Baada ya hapo wanakijiji walipisha njia. Washindi waliondoka mbio na Bibi Arusi wao kuelekea kijijini kwao. Walipokaribia kijijini waliimba wimbo uliojulikana. "Twamleta Omwenga Eeee!" (Tumemleta Bibi Arusi). Mara moja wanawake wote waliobaki nyumbani walikimbia mbio kuwalaki kwa nyimbo na vigelele. Bibi Arusi sasa alishushwa kutoka kwenye baiskeli akabebwa mabegani na mwanaume mmoja mwenye nguvu. Walipofika nyumbani alimtua chini polepole, akaelekezwa kwenye nyumba ya mmewe hali ushunu wa shanga umefunika uso wake. Usiku huo ngoma zilianza kwa nguvu nao wazazi wa Bwana Arusi wakijigamba uwanjani. Bibi Arusi alikutwa bikira. Kesho yake ng'ombe wengine walipelekwa kwa wazazi wake kama shukrani ya malezi bora. Ngoma zilichezwa siku tatu. Bibi Arusi hakuonekana mpaka siku ya tatu, siku ya kupewa zawadi na ndugu wa Bwana Arusi na wanakijiji. Siku hiyo ushungi ulifunuliwa. Wanakijiji walipomwona walisema, "kweli mwanamke ndiye huyu!" Uzuri wake uliwatia kiwewe ilisemekana huyo binti aliwakataa wachumba wengi waliopeleka posa. Wanakijiji wakampa jina la "Lutezya Balenzi" (Mkataa Wampenda), yule binti wa hadithini aliyewakataa wachumba wengi. Kwa kifupi jina lake likawa "Balenzi." Jina lake la "Mkaya" likafa.

Hayo yamepita.

Leo ni Jumamosi. "Hatutaki fujo hapa!" mzee mmoja alifoka. "Enanga ni chombo cha kusikilizwa kwa makini! Kama unataka kupiga kelele nenda kacheze zeze huko kwenye mashindano ya ngoma!" Huyo alikuwa Mzee Bakaraza, mzee aliyejulikana kijinini kwa busara yake.

"Hiki ni chombo cha maneno mazito!" mzee mwininge aliongezea. Wazee walikuwa wamekaa kuuzunguka mtungi wa pombe ya ndizi (emphahe au olubisi). Mzee Zikambona alikuwa amekaa katikati karibu na mtungi, enanga yake ikiwa pemberi mwa debe shinda liliosaidia kuongeza sauti. Wazee waliskiliza kwa makini kila neno, likatua vizuri miyoni mwao. Aliimba kwanza nyimbo rasmi zilizojulikana kama "Amalende, Gaude, Lukumbuzya akaza mwisoma (Lukumbuzya alikwenda kusoma) na zingine za kale. Kila baada ya wimbo mgawaji wa pombe alipitisha mzunguko wa pombe mmoja au miwili kufuatana na urefu wa wimbo. Baada ya hizo nyimbo alipiga wimbo wake mpya. Uliwashangaza sana wasikilizaji. Waliguna tu wakiwa wameshika matama. Waliomba upigwe tena na tena. Wimbo huo waliupa jina la "Balenzi." Wazee walitawanyika usiku wa manane kwenda majumbani kwao walipoona dalili za mvua kunyesha. Mzee Zikambona na

mkewe waliyumbayumba wameshikana mikono kuelekea kwenye nyumba yao. Waliangukaanguka pamoja na kusaidiana kusimama hadi walipofika. Walipofika nyumbani Balenzi alimwambia mmewe. "Mume wangu! Naona kama mchungwa haupo!"

Balenzi, umekunywa pombe kiasi gani," mmewe alimjibu. "Pika haraka tule tulale." Balenzi alipika haraka wakala, wakalala kwenye upweke ambaa ulikuwa blanketi lao.

### **Na kwa nini wasikumbuke?**

"Bantumwe! Shangilieni!" mwanamke mmoja kijijini alipiga vigelegele akipeperusha khanga yake hewani. "Bantumwe" Asiyé na mtoto aeleke jiwe! Mwenye upweke avute blanketi lake! Antoni Lukonge alikuwa huko mbele karibu na meza ya wazazi wake akitoa hotuba ya kuwashukuru. Wazazi wake walikuwa wamefikisha miaka ishirini na tano ya ndoa. Antoni, mtoto wao pekee aliwafanya sherhe kubwa ambayo ilikuja kukumbukwa sana kijijini. Watu walikuwa wamekwisha kula na pombe ilikuwa sasa ikigawiwa kwa watu waliokuwa wamekaa katika duara ndogo ndogo. Kila kikundi cha watu na mtungi wake katikati. Antoni aliendelea na hotuba.

"Mtoto, hata awe na cheo kikubwa namna gani hawezi kuzidi bega la mzazi wake. Kwa heshima na unyenyekevu ninatoa shukrani kwa wazazi wangu. Bila wao nisingkuwa kama nilivyo."

Vigelegele vilifuata. Ilikuwa hotuba ambayo iligusa mioyo ya wazazi wengi. Baada ya hotuba kilifuata kitendo cha kukata keki iliyokuwa na mishumaa ishirini na mitano. Wanakijiji walikuwa hawajapata kuona kitu kama hiki. Maelezo yalitolewa kuhusu maana ya mishumaa. Baada ya hapo Mzee Lukonge na mkewe waliombwa kuzima mishumaa hiyo kwa mkupuo mmoja wa pumzi. Hawakuweza kuizima yote. Mishumaa miwili ilibaki ikiwaka. Walimalizia. Walikata keki na kisha mtoto wao akawalisha kipande, mmoja mmoja. Sherehe ziliendelea kwa ngoma za Mganga Gholita hadi usiku wa manane. Yote haya yalikuwa wazi hasa kwa watoto waliokumbuka keki kulio kitu kingine. Watoto hawa walikuwa sasa mashulenii wakifuata nyayo za Antoni aliywetia hamasa ya kusoma.

Jumapili hii watoto kijijini walikuwa na dukuduku la kumwona "Nyokonyoko." Walikuwa na hamu ya kujua kama amesalimika na kusikia maneno yake juu ya mvua ya usiku, kwani usiku huo mvua ambayo ilikuwa haijapata kuonekana kwa miaka mingi ilinyesha usiku mzima. Ilianza kukatika kwenye majira ya saa nne hivi. Ng'ombe ambaa walikuwa hawajakamuliwa au kufunguliwa zizi walikuwa wakililia, nao mbuzi waliweka mahadhi yenyé mtetemeko kwenye anga lililokuwa limetawaliwa na kimya. Wanakijiji ambaa walikuwa bado na blanketi zao walitoka nje kuchungulia jua lililokuwa likitokeza kiuficho mawinguni. Watoto walionekana wakiruka mifereji ya maji wakielekea nyumbani kwa Mzee Zikambona. Hawakumkuta amekaa chini ya mchungwa kama kawaida yake. Nyumba ilikuwa imefungwa bado.

Walifikiri labda ni mojawapo ya michezo ya Balenzi. Walikwenda kwenye mlango wakagonga kwa kelele. "Nyokonyoko! Zikambona! Nyokonyoko!" Hapakuwa na jibu kutoka ndani. Walijaribu kuusukuma mlango, lakini ulikuwa umefungwa kwa ndani. Watoto walitawanyika mbio kwenda kuwaeleza wazazi wao. Kila mmoja alisema lake. Wanakijiji walistuka. Walikwenda kwa haraka nyumbani kwa Mzee Zikambona. Wallita. Hapakuwa na jibu. Mlango ulikuwa mgumu. Walivunja dirisha la mbao na mwenzao mmoja akapita kuingia ndani. Aliyeingia aliona, akastuka, akawafunglia wengine mlango. Waliingia kwanza wazee watatu. Baada ya muda walitoka njekuwaeleza wenzao kilichotokea. Maelezo yalikuwa mafupi. Mzee Zikambona alikuwa amemkumbatia mkewe. Uso wake ulionyesha michirizi miembamba ya machozi yaliyokauka. Machozi ya uzeeni. Enanga yake ilikuwa karibu naye. Wanakijiji sasa waliduewa wimbo mpya. Habari zilipelekwa kwa ndugu zao. Kesho yake jioni wakazikwa kaburi moja karibu na mchungwa. Kijijini kaburi lao likawa kumbukumbu ya wapendanao katika mema na majonzi.

Katika mji huu wa Mzee Zikambona na mkewe Balenzi kulikuwa na mwangwi wa sauti uliozungukazunguka.

"Mwanangu! Kwa nini unasema hutaki mizigo?" mama yake alisema kwa kunung'unika hali akifungasha mchele, viazi vilivyochoomwa, samaki wakavu machungwa, ndizi, mihogo, nab ado mama yake alikuwa akisomba vitu vingine kutoka ndani ya nyumba.

"Mama, huko Dar es salaam pia kuna vyakula!" Antoni alikaa kimya. Alijua mama yake akifanya kitu mpaka moyo wake mwenyewe uridhike. Ilikuwa siku yake ya kurudi kazini. Alikuwa amekuja kumalizia nyumba ambayo alikuwa akiwajengea wazazi wake. Ilikuwa nyumba ya kwanza ya batii kijijini. Siku hiyo wazazi wake walimsindikiza mtoto wao hadi Nansio kwenye boti. Balenzi alitokwa na machozi alipoona boti inatega mgongo kuelekea Mwanza. Waliporudi nyumbani walifungua radio kwa hamu kusikiliza habari. Mtoto wao Antoni alikuwa amewaletea zawadi. Habari zilieleza kuwa majeshi ya nchi jirani yalikuwa yameteka sehamu ya Tanzania. Balenzi alistuka. Usiku huo hakulala. Kesho yake asubuhi Balenzi alikuwa wa kwanza kuamka. Alianza kufagia uwanja wa pale nyumbani. Wakati anafagia karibu na mchungwa aliona mchwa umeanza kujenga kwenye shina lake. Kwa haraka aliutoa, akatifua kidogo kwenye shina kisha akamwagia maji ya moto. Kila siku akawa anauchunga.

Jumamosi hiyo Balenzi alichimba mihogo akiwa na mawazo mengi. Moyo wake ulikuwa na majonzi mengi. Mikono yake ikawa mizito. Mara mbili karibu ajikate jembe na wakati fulani karibu achomwe na kijiti jichoni. Balenzi aliona hakuwa katika hali yenye makini. Hata nusu kikapu hakujaza. Alirudi nyumbani kupika chakula cha mchana. Alimkuta mmewe ametandika mkeka chini ya kivuli cha mchungwa, amelala na enanga yake kifuani. Alimwacha kama alivyokuwa, akaingia ndani ya nyumba kupika.

Wakati akipika aliyakumbuka tena maneno aliyoambiwa na mmewe usiku uliopita, maneno ambayo yaliibua kumbukumbu na kuvuruga majonzi mazito yaliyokuwa chini ya mtungi wa upweke wao. Maneno hayo yaliwasumbua wote wawili siku hiyo. Ni kweli kesho yake wangetimiza miaka hamsini ya ndoa yao. Machozi yalimlengalenga, yakadondoka motoni alipoinama kusukuma kuni zilizokuwa zikiwaka pemberi. Machozi sasa yalitoka kwa wingi. Akaweka viganja vyote viwili machoni. Alipovitoa mikono yote ikawa imeloana. Alipigapiga vidole, machozi yakasambaa kisha akajipangusa kwenye nguo yake mbavuni. Alijikaza akamaliza kupika---ugali kidogo, viazi vitamu vilivyopikwa na maganda yake, na samaki aina ya sato, pamoja na vijibuyu vidogo vya maziwa. Alimwamsha mmewe wakala pamoja chini ya kivuli cha mchungwa.

Kimya.

“Balenzi,” mmewe alisema baada ya kumeza tonge moja la ugali. “Naona macho yako mekundu. Ulikuwa ukilia?”

“Mume wangu! Hayo si ya kusema.”

“Ni kweli. Hata mimi hali yangu si nzuri. Nilipokuwa usingizini niliota tukiwa vijana.”

“Tulikuwa na umri gani”

“Arusi yetu. Yote yalikuwa wazi.”

“Naona mwenzagu fikra zako zinarudi nyuma kwenye mazuri. Mimi zangu zinarudi kwenye mabaya tu, na nikifiria ya mbele yanaishia kesho.”

Kimya.

“Mume wangu! Ni kweli kuwa ng’ombe wa maskini hazai?”

“Balenzi, hayo si ya kusemwa.”

Wakati huo waliskia mtu akibisha hodi. Alikuwa Mama Bantumwe. Wanakijiji walimpa jina hilo la “Bantumwe” yaani “Enyi watu!” kwa sababu alikuwa na mazoea ya kuita watu “Bantumwe!” Utamsikia akisema, “Bantumwe! Ebu leteni kuni! Bantumwe! Acheni kunichekeshal!” Hata alipokuwa akishangaa alisema, “Bantumweeee!”

“Bantumwe! Ninyi ndo sasa mnakula!”

“Acha maneno, karibu nawa mikono,” alisema Balenzi.

Alinawa wakala pamoja.

“Watu huko wameanza kuimba, ninyi bado mko hapa. Malizeni haraka twende.”

“Mzee Barakaza leo vipi?” aliuliza Zikambona.

“Leo katoa pombe safi ya ndizi. Imeiva vizuri hasa! Natoka huko sasa hivi. Watu wanasubiri enanga yako tu unywaji unoge. Wamehimiza lazima nirudi nanyi.

Walimalizia kula, wakafunga nyumba na wote watatu wakaongozana kuelekea kwa Mzee Bakaraza, Mzee Zikambona akiwa na enanga yake kwapani. Huko ndiko alikopiga wimbo wake mpya na enanga yake ya mwisho. Walirudi nyumbani usiku, dalili za mvua zilipanza kuonekana. Hawakuliona jua la Jumapili. Siku yao ya kutimiza miaka hamsini ya ndoa.

Ilikuwa asubuhi kama saa mbili hivi. Hii ndiyo ilikuwa siku ya siku. Siku ilioanza kung'oa moyo na mizizi yake. Ilikuwa siku ya Jumamosi. Walimkuta Mzee Lukonge amekaa chini ya mti wa mchungwa. Walimweleza. Akainamisha kichwa chini kwa muda mrefu kidogo, kasha aliinuka akatembea hatua chache akamwita mkewe ambaye alikuwa akianika udaga kwenye jiwe nyuma kidogo na nyumba yao alipokuja alimkuta mmewe ameinama kichwa chini. "Mwelezeni," Mzee Lukonge aliwaambia. Walianza kwa kumwuliza kama ye ye ndiye alikuwa Mama Antoni. Akakubali. Kisha wakaeleza sifa za mwanae huko jeshini, jinsi alivyopanda haraka, na jinsi Taifa liliyokuwa likimwenzi. Alianza kuhisi

"Ebu nambieni! Mwanangu amefariki dunia!" walisita. "nambieni!" wakatoa taarifa kamili waliyokuja nayo.

Kilio kilichotoka hapo kiliwainua wanakijiji, hata waliokuwa mashambani tayari waliacha majembe yao. Bantumwe alikuwa wa kwanza kufika. Akamshika Balenzi kiubavuubavu akampeleka ndani ya nyumba. Mara Mzee Bakaraza na wengine wakawa wamefika. Wale watu wawili ambao walisema ni wanajeshi waliwaeleza wanakijiji kwa kirefu. Wakamalizia kwa kusema kuwa ndege yenyen maiti ingefika asubuhi hiyo saa nne. Waliwahimiza watu waanze kuongozana kwenda uwanjani. Watu walianza kuelekeea huko. Walimwomba Bantumwe na wanawake wengine wawili wabaki nyumbani na mfiwa.

Saa nne kamili mlion wa ndege ulianza kusikika. Balenzi alianza kutetemeka mwili mzima. Mlio ulipokaribia, ghafila alikurupuka akatoka nje kuitazama ndege. Akaiona inaanza kutua.

"Namwona mwanangu!" alipiga kelele. Nguvu zikamwishia.

"Bantumwe! Nisaidieni!" Bantumwe alisema alipomwona anaanza kupepesuka. Alizimia. Alipelekwa nyuma ya nyumba upenuni wakaanza kumpepea kwa khanga. Mazishi yalikuwa Jumapili kesho yake kwenye kaburi la kanisa. Baada ya mwaka mmoja Balenzi alianza huo ugonjwa wa kila Jumamosi kufukuzana na ndege na kuitukana. Wazee hawa wawili wakaanza kushikamana kiajabu. Wakawa pia na mapenzi ya izeeni ya aina ya pekee. Mdomoni mwa Balenzi maneno "Mume wangu" yakawa hayamwishi. Mzee Lukonge akatunga wimbo mpya wa enanga. Akauita "Zikambona." Wimbo huu ulikuwa juu ya kifo cha mwanae pekee, na ukiwa wake na mkewe. Wimbo ukawasikitisha sana watu wengi. Kila ulipopigwa ukawa unawaliza wasikilizaji. Wanakijiji wakamwita Lukonge, Zikambona. Jina la Lukonge likafa. Wanakijiji wakawapenda hawa wazee wawili, nao watoto kijijini wakuona mji wa Zikambona kama wao.

Nani ajuaye uchungu waliokufa nao hawa wazee wawili? Iulizeni mihogo iliyozunguka nyumba yao. Haitakupa jibu. Wadudu wanaotambaa na kuruka pale nyumbani hawana jibu. Nani atakwambia siri ya mchungwa na kivuli kilichowasitiri wazee hawa? Nyuki walioyazungukia maua yake hawajui. Watoto waliozoea kuchuma matunda yake hawakuona unapandwa.

Ni mtu mmoja tu pale kijijini akumbukae bado. Mtu huyu ni Bantumwe. Ukimwuliza atakwambia.

Ilikuwa Jumamosi. Siku ambayo kwa kawaida watoto hawaendi shule. Bantumwe alikuwa amekaa na wazee hawa wawili upenuni mwa nyumba yao ya mbavu za mbwa. Ilikuwa jioni. Antoni alioneckana akija mbio nyumbani kifua wazi na mche wa mchungwa, manati yake mkononi.

“Mama! Nimekuta huu mchungwa umejotesha msituni wakati tukiwinda ndege. Eti, si mchungwa huu? Wengine wanasema eti ni mdimu.”

“Ebu ulete hapa,” baba yake alisema. Alitoa jani moja, akalipikicha kwa vidole viwili kisha akanusa. “Ni mchungwa. Kaupande pale. Labda tutapata kivuli cha kupumzikia hapo baadaye.” Antoni aliupanda. Asububi na jioni mtoto akawa anaumwagilia maji. Akakua nao.

Na nani ajuaye siri ya ng’ombe wachache waliokuwa nao kabla ya kifo chao? Wanakijiji wote wazee wanajua. Watakusimulia.

Mzee Lukonge na mkewe Balenzi waliuza ng’ombe wote waliokuwa nao kumsomesha mtoto wao pekee. Wakavaa matambara. Wakawa maskini wa kutupa. Mzee Lukonge akaanza kujifunza enanga. Akaimba juu ya umaskini wake, akapata angalau pombe ya bure. Akajifunza nyimbo rasmi za zamani, akapata sifa. Mtoto wao alipoanza kazi alitumia nusu ya mshahara wake kwa kwanza kuwanunulia ng’ombe mmoja wa kufutia kwanza uchungu wa kuuza ng’ombe wao wote. Mshahara wa pili akawavisha. Wakawa watu.

Lakini sasa tazama. Nani ajuaye siri ya haki maishani mwa binadamu? Mzee zikambona na mkewe Balenzi walijiuliza swali hili mara nyingi walipokuwa wamekaa kivilini chini ya mchungwa. Walihisi siku moja atatokea mtu kusimulia hadithi yao --- jibu lipatikane. Na likipatikana afanyiwe nini? Kuishi kuishia.

Swali la kusikitisha zaidi lilisikika siku ya mazishi ya Antoni. Baada ya wanajeshi kumaliza kutoa heshima zao, Balenzi alikwenda karibu na kaburi, akapiga magoti, mikono akaiweka kifuani ikipishana kama X, sauti ya juu iliojaa masikitiko ikamtoka.

“Nilie na nani jamani! Nilie na nani jamani!”